OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA KISARAWE
SHULE YA SEKONDARI MINAKI

**Email: minakisc@kisarawedc.go.tz**
**Website:**
**https://minakisecondaryschool.ac.tz**

**S.L.P 28004**
**Kisarawe-Pwani**

**MKUU WA SHULE - 0766361804**
**MAKAMU M/SHULE 0692 471345**
**-0752285438**
**MWANDAMIZI MALEZI - 0685697015**

**Kumb. Na. MSS.210/189**

**Kwa ………………………………………….**
**...…………………………………………..**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MINAKI HALMASHAURI YA KISARAWE MKOA WA PWANI MWAKA 2025/2026**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2025/2026 na atasoma tahasusi ya …….……

Shule ya Sekondari **MINAKI** ipo umbali wa Kilometa 2.5 Mashariki mwa Mji wa **Kisarawe** Usafiri wa basi kutoka mjini **Dar es Salaam** unapatikana katika kituo cha mabasi cha **Gongo la mboto** nauli yake ni shilingi **700**/.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **08/07/2025** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **08/07/2025** Mwisho wa kuripoti ni tarehe 22**/07/2025.** Muda wa Kuripoti ni kuanzia saa 1:30 Asubuhi mpaka saa 10:30 Jioni

**SENI K. MAHEGA**
**MKUU WA SHULE**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

**2.1. Sare za Shule**

i. Sare ya shule ni Suruali **Nyeusi** (***Suruali mbili***). Maelezo ya mshono (**Suruali ya rangi nyeusi (plain black) isiyo na alama yoyote, iwe ya heshima, Marinda mawili kila upande kwa mbele, mifuko ya mbele iwe miwili (mmoja kila upande) na isiwe kama ya suruali ya jeans, isiwe ya kubana /chupa na upana wa chini uwe kuanzia sentimita 17 na pindo za chini za suruali zikunjwe kwa nje (iwe na turn up)-Unaweza kupata kwenye maduka yaliyopo karibu na shule.**

ii. Sharti nyeupe mikono mifupi lenye mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto lisilo bana mwili na urefu wa kutosha kuchomekea. mikono mifupi (***sharti mbili***);

iii. Sare ya Michezo ni Bukta na fulana **ya Blue**

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili na zaidi nyeusi za shule;

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta **nyeusi**,moja

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali za **rangi ya kijivu** (dark grey) jozi mbili **yenye mshono sawa na ile sare ya shule.** Nguo zingine hazitaruhusiwa kuvaliwa shuleni hivyo **usilete nguo za nyumbani**.

xi. Tisheti (T-shirt) ya Form six rangi ya **Dark Blue** yenye kola na Nembo ya Shule. Jozi mbili (2).

**Aidha suruali ya dark grey, tisheti na sweta nyeusi, unaweza kuvipata kwenye maduka yaliyopo karibu na shule**

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari Kaunta book (**Quire 3 au 4**) mawili kila somo

ii. **Ream** paper **moja (1)** A4 aina ya **DOUBLE A**, Pamoja na Ruled Paper **moja (1)**

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma **Biology; (PCB & CBG)**

v. Scientific Calculator (fx-991-ES PLUS) na Graph pads mbili (02) kwa wanafunzi wanaosoma **PCM, PCB, CBG, PGM, EGM na HGE.**

vi. Godoro lenye upana wa futi 2.5

vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya **pinki,** blanket 1, godoro dogo 1, chandarua 1 rangi ya **blue**

viii. Nguo za ndani za kutosha;

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe); **visiwe vya plastic.**

x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xi. Vifaa vya Usafi

| NA | TAHASUSI | AINA YA KIFAA |
|---|---|---|
| 1 | **HKL** | Fagio la chelewa refu lenye mpini na Dawa ya kudekia chooni lita 5 aina ya Super Gold,Timo au Lit na reki lenye mpini |
| 2 | **HE** | Fagio la chelewa refu lenye mpini**,** brash ndogo ya kusugulia masinki, Fyekeo, Dawa ya kudekia chooni lita 5 aina ya Care line |
| 3 | **EGM** | Fagio la chelewa refu lenye mpini, Fagio refu lenye mpira wa kukaushia maji (Squezer) na sabuni aina ya Care line. |
| 4 | **CBG** | Fagio la chelewa refu lenye mpini, Mopper , Care line na Soft broom |
| 5 | **PCB** | Hard broom, Panga, **Jembe na Mpini** |
| 6 | **PGM** | Squezer, Fyekeo, **Jembe na Mpini** |
| 7 | **PCM** | Fagio la chelewa refu lenye mpini, Fagio refu lenye brashi laini (soft broom) na Sabuni ya Maji lita 5 aina ya Tarmol |

**NB: Vitu vyote hivyo unaweza kuvipata kwenye maduka yaliyopo karibu na shule**

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**UTARATIBU WA KULIPIA;**

Shule haipokei **fedha tasilimu au hundi** kutoka kwa wazazi **/** walezi wa wanafunzi na badala yake malipo yote yaliyoanishwa kwenye jedwali hapo juu yalipwe kupitia **BENKI ya NMB** (National Microfinance Bank) kwenye tawi lililopo karibu na wewe kabla ya kuja shuleni.

Jina la Akaunti ya Shule ni: **MINAKI SECONDARY SCHOOL**

Namba ya Akaunti: **21401100002**

**2.4** ***Kikao cha Wazazi/Walezi na bodi ya shule kitaambatana na Visiting day kwa muhula wa kwanza itakuwa tarehe 18/10/2025.***

**Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.0. Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Night preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini awapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.**

**3.1 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na miongozo ya serikali;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule na itaharibiwa**;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
**xviii. Kumiliki na kutumia Redio, Pasi, na kifaa chochote kinachotumia umeme mfano chaja, earphone n.k.**

**4. AFYA** Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na bima ya Afya yoyote,Kama hana bima ya afya anatakiwa kuja shuleni **na Kiasi Cha Tsh 50,400/= kwa ajili ya kukata bima ya afya ya NHIF.**

**5. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule
iv. Picha mbili za mwanafunzi na picha (3) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Cheti cha kuzaliwa
vi. Result slip na leaving certificate ya kidato cha nne
vii. Sanduku imara la chuma la kuhifadhi mali yake binafsi (tranka)

**6.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MINAKI**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………….**
**Jina la Mkuu wa Shule ………......................................**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule - 0766 361804**
- **Makamu Mkuu wa Shule - 0692 471345**
  **- 0752285438**
- **Mwandamizi Taaluma - 0784833854**
- **Mwandamizi Malezi- 0685697015**

## ORODHA YA VITABU

**VIFUATAVYO NI BAADHI YA VITABU VINAVYOTUMIKA SHULENI**

Mwanafunzi anashauriwa kununua vitabu kulingana na masomo yake kwa kufuata mchanganuo ufuatao.

| **CHEMISTRY** | **GENERAL STUDIES** | **HISTORY** | **KISWAHILI** |
|---|---|---|---|
| 1. Modern's ABC of Chemistry by Dr. s. Jauhar (2017-2018) for class XI & XII part I & II<br>2. Essentials of Physical Chemistry class XI & XII by Chand<br>3. Advanced Physical Chemistry by Ngaiza Lusima (2014)<br>4. Conceptual Chemistry for Class XI by S.K JAIN<br>5. Comprehensive Chemistry volume I class XII by Dr. N.K. Verma, S.K. Khanna & Dr. B. Kapila<br>6. Advanced Organic Chemistry by Arun Bahl, S. Chand | 1. Understanding General Studies For Advanced level (5&6) by Joannes Bigirwamungu & Sospeter M. Deogratius<br>2. General Studies Alive (5&6) by Zisti Kamili (2017)<br>3. General Studies Notes: Current syllabus Approach form 5&6 by Nyambari Nyangwine, G.M Zombwe, Godfrey Mshiu & James Egino | 1. Advanced Learning World History by Idrisa Msuya book 1 & 2<br>2. Essentials in Advanced level History paper 1 & 2 by Saleh Yasin<br>3. Advanced Level History 1 & 2 by K. Shibitali<br>4. Medieval Ages paper 2 by M Mavunde | a) USHAIRI<br>1. Kimbunga by Haji Gora (TUKI)<br>2. Chungu Tamu by T. A Mvungi TPH Ltd<br>3. Fungate ya Uhuru by Mohamed Seif Khatibu (Macmillan Aidan Ltd)<br>4. Mapenzi Bora by Shaaban Robert, Mkuki & Nyota publishers<br>b) RIWAYA<br>1. Mfadhili by Hussein Tuwa, Macmillan Aidan Ltd<br>2. Vuta n'kuvute by Shafi A. Shafi, Mkuki & Nyota Ltd<br>3. Usiku Utakapokwisha by Mbunda Msokile, Macmillan Aidan Ltd<br>4. Kufikirika by Shaaban Robert, Mkuki & Nyota Ltd<br>c) **TAMTHILIYA**<br>1. Kivuli Kinaishi by Said Mohamed, Oxford University Press<br>2. Morani by E. Mbogo, Macmillan Aidan Ltd<br>3. Kwenye Ukingo wa Thim by Ebrahim Hussein, Oxford University Press<br>4. Nguzo Mama by Penina Mhando, Macmillan Aidan Ltd |
| **ADVANCED MATHEMATICS** | **BASIC APPILED MATHEMATICS** | **GEOGRAPHY** | |
| 1. Advanced Mathematics for Advanced Level Secondary Schools form five by TIE<br>2. Advanced Mathematics for Advanced Level Secondary Schools form Six by TIE<br>3. Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools Form V & VI by Septine I. Sillem (2015)<br>4. Conceptual Advanced Mathematics For Secondary Schools Form V & VI by P. L. Mayombya | 1. Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools form V by Septine I. Sillem, 2014<br>2. Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools form VI by Septine I. Sillem, 2014<br>3. Basic Applied Mathematics for Advanced Level Secondary Schools form five and Six by TIE | 1. Integrated Approach in Geography by David Waugh (2009) 3rd edition<br>2. A Comprehensive Approach in Physical Geography by D.T. Msabila (2018)<br>3. Practical Geography by Zisti Kamili 2nd Edition 2016<br>4. Complementary Physical Geography for secondary school by O. Mpalaki & F. Lighuda 5.Affordable Edition for Advanced learners by Zist Kamili | |

| **ENGLISH LANGUAGE** | **ECONOMICS** | **PHYSICS** | **KISWAHILI 1 & 2** |
|---|---|---|---|
| 1. Advanced level English Language 1 by Ndambo, NNP Publishers<br>2. Advanced English Language form 5&6 by James John, Oxford university press<br>3. English language for secondary school, language and use form 5&6 by TIE<br>4. Advanced level English language form 5&6 by Nicholous Asheli<br>5. Oxford Advanced learners Dictionary by Oxford university press<br>6. Betrayal in the city by Francis Imbunga, East African Education publishers<br>7. The Beautiful ones are not yet Born by Ayi Kwei Armah. Heinemann Educational Publishers 8. A man of the people by Chinua Achebe. Heinemann Educational Publishers<br>9. An Enemy of the people by Henrick Ibsen. East African Educational Publishers<br>10. Black Mamba by John Ruganda<br>11. I will Mary when I want by Ngugi wa Thiong'o and Ngugi wa Mirii<br>His Excellency The head of State by Danny Safo. Macmillan Publishers limited<br>12. Selected Poems by TIE<br>13. The Wonderful Surgeon and other Poems by Charles Mloka<br>14. A Season of Waiting by David Omowale. East African Educational Publishers | 1. Economics 1 & 2 by Tayebwa Mgisha<br>2. Modern Economics Theory by Dewelt.<br>3. Essential Economics 1&2 by Odhiambo.<br>4. Modern Economics 20th Edition by Ahuja<br>5. Comprehensive of Economics Questions and Answers by Tayebwa.<br><br>**BIOLOGY**<br>1. Biological science(D) Taylor,N.Green<br>2. Advanced Biology,(By C.J.Cleggy) 3.New understanding Biology (Glenn and Susan Toole | 1. Physics for Advanced level secondary schools, students book Form five by TIE<br>2. Physics for Advanced level secondary schools, students book Form six by TIE<br>3. Principles of physics for class XI, V.K Mehta, S. Chand<br>4. Principles of physics for class XII, V.K Mehta, S. Chand<br>5. Modern ABC of physics for class XI part I & II by Satish K. Gupta<br>6. Modern ABC of physics for class XII part I & II by Satish K. Gupta | 1. Nadharia ya Fasihi by Kilangi Enock Lucas, Zenur Printers Dsalaam 2019<br>2. Tahakiki ya Kiswahili by Kilangi Enock Lucas, Zenur Printers Dar es salaam 2019<br>3. Kiswahili 1 kwa Shule za Sekondari kidato cha 5 & 6 by Kilangi Enock Lucas, Zenur Printers Dar es salaam 2019<br>**KISWAHILI 1 & 2**<br>4. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) sekondari na vyuo by Y.M Kihore, Massamba na Msanjila, TUKI<br>5. Kitangulizi cha Tafsiri Nadharia na mbinu by H.J Mwansoko, Mekacha na Mtesingwa, TUKI |

**NB: Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na kitabu kimoja kwa kila somo la tahasusi yake, hivyo inashauriwa pia kila mwanafunzi anunue vitabu vya Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) na Vitakaguliwa siku ya kuripoti shuleni.**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**
SHULE YA SEKONDARI MINAKI
**FOMU YA TAARIFA ZA MWANAFUNZI** **MSS.K5. A**

**1.** Jina lako kamili………………………………………………
**2.** Kidato ulichojiunga hapa shuleni……………………. mchepuo…………………
**3.** Jina la mzazi/mlezi…………………………………………
Anuani yake………………………. Simu ya ofisini ya mzazi/mlezi……………………………. simu ya mkononi ya mzazi/mlezi……………………………….
Kazi yake…………………………………………….

**4.** Mahali ulipozaliwa
(i) Mkoa……………………… Wilaya ………………… Kata……………
(ii) Tarafa……………………… Kijiji cha …………………………..
(iii) Tarehe ya kuzaliwa.…………………………………………….
**5.** Mahali unapoishi sasa……………………………………
Anuani yako………………………………………………….
**6.** Dini/dhehebu lako……………………….
**7.** Unaishi na Baba tu/mama tu/wazazi wote/mlezi…………………………….

**8.** Kama unalelewa an mlezi asiye mzazi wako
Jina la mlezi wako (Majina matatu)……………………………………………..
Uhusiano na mlezi wako (Kaka, dada, n.k)………………………………………..
Anwani yake …………………………… Makazi yake………………….simu…………………

**9.** i. Jina la shule ya msingi uliyosoma……………………………
Shule ya msingi ya ………………………………Anuani………………………….
ii. Jina la shule ya sekondari uliyosoma………………………………………………....
……………………………………Anuani………………………………………….

**10.** Michezo unayocheza
(a)…………………………………
(b) …………………………………

**11.** Vyama vya kujifunza ambavyo wewe unapenda kuwa mwanachama:
Scout, Fema, Wapinga Rushwa(PCCB), Mali Hai, Ant Aids, School Magazine na Mazingira.
(a)……………………………………………..
(b)……………………………………………
(c)………………………………………………
**12.** Je unao ulemavu wowote? (Ndiyo / Hapana)
Kama Ndiyo taja aina ya ulemavu……………………………………………………..

**NB:** Mazingira ya shule si rafiki kwa watoto wenye ulemavu.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**
SHULE YA SEKONDARI MINAKI

**FOMU YA UTHIBITISHO** **MSS.K5. B**

Fomu hii ijazwe na mzazi au mlezi wa mwanafunzi katika sehemu zake na irudishwe shuleni ikiwa imeambatanishwa na picha ya mzazi/mlezi. Shule itatoa taarifa kwa mzazi / mlezi ambaye picha yake na maelezo yake yataonekana katika fomu hii.

Mimi…………………………………………………mzazi/mlezi wa Mtoto wangu……………………………………nimeona, nimeelewa na nimekubali masharti yote yanayohusu mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari ya Minaki. Nitampa mahitaji yote yanayotakiwa na nitashirikiana na walimu wa shule ya Minaki katika kumlea vizuri mtoto wangu ili aweze kusoma na kuelewa na hatimaye aweze kufanya mitihani yote ya ndani shuleni na ya Taifa kwa mujibu wa ratiba.

Saini ya mzazi/mlezi………………….

Anuani ya mzazi/mlezi

………………………..

……………………………

Simu………………………

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI:**

Mimi…………………………………………… mzazi/mlezi wa mwanafunzi……………………………………………wa kidato cha tano.

Nakiri kwamba yaliyoandikwa hapo juu kwenye fomu zote mbili (MSS.K5. A na MSS.K5. B) ni sahihi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina…..…………………….** | **Jina …………………** | **Ndugu** | **Ndugu** |
| Picha ya Mwanafunzi | Picha ya Mzazi/Mlezi | Jina…………………...<br>Uhusiano………………<br>**Namba ya Simu…………** | Jina…………………...<br>Uhusiano………………<br>**Namba ya Simu………** |

**SAINI YA MZAZI/ MLEZI.**

……………………

Tarehe………………………

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**
SHULE YA SEKONDARI MINAKI

**FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA** **MSS.K5.ME**
(Request for Medical Examination)

This form is to be completed by a Medical Officer (*Government Hospital*)

**Name of Student…**…………………………… **Age:** ……... **Sex:** …………

The above named has been examined in respect of:

**(a) STOOL** **………………………………………………………………………**

**(b) URINE ...……………………………………………………………………**

**(c) CHEST** **…………………………………………….....................................**

**(d) BLOOD ……………………………………………………………………….**

**(e) EYES** **……………………………………………………………………………**

**(f) EARS** **……………………………………………………………………………**

**(g) HEART** **……………………………………………………………………...**

**(h) STOMACH ULCERS** **……………………………………………………...**

**(i) OTHERS** **…………………………………………………………………….**

I am satisfied / not satisfied that the above named Student is physically and mentally fit to pursue further studies in Secondary School.

**………………………………** **………………**
**SIGNATURE (and official stamp)** **DATE**

**………………………** **……………….**
**DESIGNATION** **STATION**

**N.B.** Fomu hii ijazwe na Daktari wa Hospitali ya Serikali (na sio hospitali ya Binafsi). Mwanafunzi anaporipoti ataikabidhi ofisi ya malezi.

TAMKO LA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI:

Nakubaliana kufuata taratibu na sheria za shule kama zilivyoainishwa hapo juu.

**JINA MWANAFUNZI…………..…………….** **JINA LA MZAZI/MLEZI…….……………..**

**TAREHE ………..…………………………….** **TAREHE ………………………………….**

**SAINI YA MWANAFUNZI……………………** **SAINI YA MZAZI/MLEZI………………….**